

Ujitokezaji wa Uradidi katika Lugha ya Kihaya: Uchunguzi wa Kategoria ya Vitenzi, Vielezi na Vivumishi

Editha Adolph
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere

Ikisiri

Makala haya yanachunguza uradidi unavyojoitokeza katika lugha ya Kihaya kwa kuangazia kategoria ya vitenzi, vielezi na vivumishi. Mtafiti amekusanya data ya makala haya katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Muleba Kata ya Izigo. Ameteua kata hii kwani ndiko inakozungamzwa Lahaja ya Kihamba inayoshughulikiwa na mtafiti wa makala haya. Halikadhalika, Kihaya kinatumiwa katika mawasiliano ya kawaida na shughuli nyingine nyingi za kiuchumi, kijamii nakadhalika. Mtafiti amekusanya data kwa kutumia mbini za hojaji na uchambuzi wa matini. Mbini ya kuchambua matini iliyotumika ni ile ya usomaji wa nyaraka za kitaaluma zilizompa mtafiti wigo wa kupata data faafu. Nyaraka zilizosomwa ni kama vile: tasnifu na maandiko mbalimbali. Hojaji hurejelea orodha ya maswali na maelekezo alioanda mtafiti ambayo hujibiwa na watafatiwa, kwa lengo la kukusanya data faafu ya utafiti. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mikabala ya maelezo na ufanuzi. Aidha, makala haya yameongozwa na Nadharia ya Uelekeani iliyoasisiwa na McCarthy na Prince (1993, 1994a, 1994b na 1995). Matokeo ya makala haya yanaonesha kuwa uradidi hujitokeza katika kategoria za vitenzi, vielezi na vivumishi katika lugha ya Kihaya. Uradidi huo huweza kuhusisha neno zima au sehemu tu ya neno. Kwa vile makala haya yamechunguza sehemu tu ya uradidi katika lugha ya Kihaya, inapendekezwa utafiti ufanyike kuhusiana na kategoria nyinginezo kama vile nomino, vihusishi, vihishishi, viwakilishi nakadhalika.

Maneno Muhimu: Uelekeani, Uradidi, Vitenzi, Vielezi na Vivumishi

Utangulizi

Dhana ya uradidi imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali. Ashton (1947) amechunguza matumizi ya uradidi na kusema kuwa uradidi hutumika kutilia mkazo jambo, kupunguza mkazo wa jambo fulani, kuonesha mueneo wa jambo pamoja na kuonesha mwendelezo wa jambo fulani. Marvcik (1978) anafafanua dhana hii kuwa ili tungo yoyote iwe radidi lazima iwe na matokeo angalau mawili ya umbo lilelile. Kapinga (1983) ametoa mifano ya vielezi vikariri vinavyofafanua vitenzi kwa kutaja kitu kilekile mara mbili mathalani, *safu safu*. Rubanza (1996a) kwa upande wake, anafasili dhana ya uradidi kuwa ni kurudufu au kurudia maneno. Neno zima linearudiwa au sehemu ya neno hilo. Aidha yapo maneno ambayo kwa mwonekeno wake hufikiriwa kuwa yamefanyiwa uradidi, ukweli ni kwamba hayana uradidi ndani yake. Rubanza (1996a) anatoa mifano ya maneno kama vile *kizunguzungu*, *barabara* na (*kulowa*) *chepechepe*. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu ni kuwa maneno haya hayana hadhi ya uradidi ndani yake kwani si kila urudiaji wa silabi ni uradidi. Maneno hayo hayarandani kikamilifu na fasili ya uradidi. Neno *chepechepe* halitokani na neno *chepe* kwani neno *chepe* linamaanisha 1. Mtu mwenye kuchekesha ama kwa mwenendo au maneno yake, 2. humaanisha mkosa, mtu asiyewafikiria na kuwajali wenzake, mtu asiyi na staha. Kwa hiyo, neno *chepechepe* halitokani na neno *chepe* kwani neno *chepechepe* linamaanisha kitu kuloa maji kwa kiasi kikubwa ambapo kwa asili neno hilo linatokana na neno *chapachapa*. Mfano mwingine ni neno *barabara* inabidi litokane na neno *bara* ambalo maana yake ni nchi kavu. Tukiangalia neno *barabara* lenye maana ya: 1. Sawasawa na 2. Njia, kwa hakika halitokani na neno hilo ‘*bara*’ lenye kumaanisha nchi kavu na silo linalorudiwa kuwa neno *barabara*. Aidha neno *kizunguzungu* inabidi litokane na neno ‘*zungu*’ lakini neno hili halina maana yoyote katika lugha ya Kiswahili. Lodhi (2004) na Ashton

(1947) kwa upande wao wamejadili dhima za uradidi kisemantiki. Lodhi amechunguza zaidi uradidi katika lahaja za Kusini mwa Unguja.

Kwa mujibu wa O'Grady na Archibald (2000) na Frawley (2003) uradidi ni mchakato wa uundaji wa maneno ambapo sehemu ya neno au neno zima hurudiwa ili kuunda neno jipya au kuongeza maana fulani ya kisarufi. Bjorkman (2009) kwa upande wake amechunguza uradidi wa vitenzi katika lugha ya Kinande. Data ya utafiti wake inadhahirisha kuwa lugha hii ina uradidi katika kategoria ya vitenzi. Bjorkman anajadili kwa kusema kuwa kiradidiwa kina silabi mbili nacho hujitokeza upande wa kushoto wa mzizi wa kitenzi na kubeba maana ya kitendo inayofanywa na kitenzi. Ili kuthibitisha ukweli huo anatoa mifano ifuatayo:

| Kinande | Kiswahili | Kinande | Kiswahili |
|----------------|--------------------|-----------------|--------------------------------|
| eri-hum-a | kuumiza | eri-huma-huma | kuumiza mara kwa mara. |
| eri-gend-a | kusafiri au kwenda | eri-genda-genda | kusafiri au kwenda kwa haraka. |
| eri-twala-a | kubeba | eri-twala-twala | kubeba kwa haraka. |

Chanzo: Bjorkman (2009)

Kipande cha data kilichopachikwa hapo juu kinathibitisha madai ya Bjorkman na kuonesha kuwa moja ya kazi ya uradidi katika vitenzi vya Kinande ni kuonesha namna ya kufanyika kwa tendo fulani kama vile tendo kufanyika kwa haraka au hufanyika mara kwa mara. Downing (2009) amechunguza uradidi wa vitenzi katika lugha ya Kixhosa na Kihehe. Utafiti wake unathibitisha kuwa katika lugha hizi, imezooleka kuwa mofimu radidiwa huwekwa kabla ya mzizi. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha pia kuwa, katika baadhi ya lugha kiradidiwa hufungamana na shina ambalo huanza na irabu au konsonanti. Utafiti huo unathibitisha zaidi kuwa vitenzi vya lugha nyingi za Kibantu vina mchakato wa uradidi nusu wa shina lake (shina la kitenzi). Mchakato huo wa uradidi huonesha maana ya kitenzi inayooonesha tendo la kufanya jambo toka wakati fulani hadi wakati fulani. Data ya utafiti wa mtaalamu huyu inaonesha kuwa katika lugha ya Kihehe kuna tofauti kati ya uradidi wa vitenzi vinavyoanza na irabu na vile vinavyoanza na konsonanti ambapo vitenzi vinavyoanza na irabu uradidi huhusisha unukuzi wa shina ikiwa ni pamoja na kiambishi kisoukomo 'kw' isipokuwa vitenzi vinavyoanza na konsonanti uradidi haunukuu kiambishi kisoukomo 'ku'. Katika lugha ya Kihehe kiradidiwa huweza kunukuu kabla na hata baada ya shina au neno. Tuangalie mifano ifuatayo kutoka lugha ya Kihehe inayothibitisha ukweli huu:

| Kitenzi cha Kihehe | Maana | Kitenzi cha Kihehe | Maana katika Kiswahili |
|---------------------------|--------------|---------------------------|-------------------------------|
| a. kú-ceénga | kujenga | kú-ceenga- ceénga | kujengajenga |
| b. kw-íimbila | kuimba | kwíimbila-kw-íimbila | kuimbaimba |
| c. kú-teléka | kupika | kú-teleka-teléka | kupikapika |
| d. kw-áaka | kuchoma | kawaka-kw-aáka | kuchomachoma |

Chanzo: Downing (2009)

Uradidi katika Kiswahili huathiri silabi, mashina ya vitenzi, maneno na vishazi, na una dhima zifuatazo: kuonesha msisitizo, kupunguza au kuongeza nguvu ya neno, kueleza hali ya kuendelea kwa tendo, au hali, na kutoa wazo la mgawanyo katika mafungu, (Mnenuka 2010). Mnenuka ameshughulikia dhima za uradidi katika Kiswahili kwa kujikita katika kategoria za kileksika. Ameangalia uradidi katika kategoria za: nomino, vivumishi, vitenzi na vielezi. Katika utafiti wake amebainisha kuwa uradidi una dhima ya kuimarisha na kudhoofisha maana. Anatoa mifano ifuatayo inayooonesha udhoofishaji wa maana unaotokana na uradidi katika vielezi vya Kiswahili:

A
 Jibril alichoma moto akiwa juu.
 Chibichi alichezea mpira katikati.
 Mawazo alilima chini.
(chini ya mlima au bondeni)
Chanzo: Mnenuka (2010)

B
 Jibril alichoma moto akiwa juu-juu.
 Chibichi alichezea mpira katikati-katikati
 Mawazo alilima chini-chini.
(chini ya mlima au bondeni).

Katika data hapo juu, mtaalamu anadhihirisha wazi kuwa uradidi uliojitokeza katika vielezi nya mahali umesababisha kudhoofika kwa maana ikilinganishwa na vile ambavyo havikufanyiwa uradidi. Anafafanua kuwa kielezi *juu* humaanisha juu kabisa na kielezi *juu-juu* maana yake ni juu kiasi. Halikadhalika, kielezi *katikati* humaanisha katikati kabisa ilhali kielezi *katikati-katikati* humaanisha katikati kiasi na kielezi *chini* humaanisha chini kabisa ilhali kielezi *chini-chini* humaanisha chini kiasi. Hivyo, vielezi vilivyoradidiwa vimedhoofisha maana ya awali.

Kipengele kingine kilichoshughulikiwa katika makala ya Mnenuka (keshatajwa) ni uimarakaji wa maana. Ili kuonesha ni kwa jinsi gani uradidi huimarisha maana katika lugha ya Kiswahili, mtaalamu huyu ameonesha mifano ifuatayo:

| A | B |
|--|---|
| Ameondoka asubuhi. Atarudi lini? Leo. | Ameondoka asubuhi. Atarudi lini? Leoleo! |
| Rhoda aliibiwa kompyuta mchana. | Rhoda aliibiwa kompyuta mchana-mchana! |
| Mlozi yule alionekana akiwanga mchana. | Mlozi yule alionekana akiwanga mchana-mchana! |
| Chanzo: Mnenuka (2010) | |

Kwa mifano hiyo ya vielezi nya wakati ni dhahiri kuwa uradidi huimarisha maana au kusisitiza jambo fulani katika lugha ya Kiswahili. Vielezi vilivyoradidiwa kama vile *leoleo* na *mchana-mchana* vinaweka msisitizo ni wakati gani jambo fulani lilitendeka au litatendeka. Wataalamu tuliowapitia hapo juu wamechunguza uradidi katika lugha mbalimbali ikiwa ni pamoja na lugha ya: Kinande, Kixhosa, Kihehe, Kiswahili pamoja na lahaja za Kusini mwa Unguja. Swali la kujiuliza hapa ni je, kuna utafiti ulioshughulikia ujitokezaji wa uradidi katika lugha ya Kihaya hususani katika kategoria ya vitenzi, vielezi na vivumishi? Jibu ni hapana. Suala hili linashughulikiwa na mtafiti wa makala haya.

Kiunzi cha Nadharia

Mtafiti anachunguza ujitokezaji wa uradidi katika lugha ya Kihaya kwa kujikita katika kategoria ya vitenzi, vielezi na vivumishi. Mtafiti ameongozwa na Nadharia ya Uelekeani iliyoasisiwa na McCarthy na Prince (1993, 1994a, 1994b na 1995). Kwa mujibu wa nadharia hii ni kuwa lazima kiradidiwa kiwe na uelekeano na kiineno au shina. Uelekeani unarejelea uhusiano wa shina na kiradidiwa. Pamoja na ukweli kuwa kiradidiwa lazima kiwe na uelekeano na kiineno au shina, ni vigumu kupata uelekeani uliokamili (McCarthy na Prince, 1993, 1994a, 1994b na 1995).

Wataalamu hawa wanapendekeza kuwa kwa vile kila lugha ina kaida na kanuni zake za uundaji wa maneno zinazojitosheleza, ni vema suala la kiini na kiradidiwa lifanyike kutegemeana na lugha husika. Aidha, kwa mujibu wa nadharia hii ni kwamba lazima uadilifu uzingatiwe wakati wa ufanyakaji wa mchakato wa uradidi kati ya umbo lisilo radidi na umbo radidiwa ili kuwepo na uelekeani kati ya umboghafi na umbotokeo kulingana na kaida, sheria na taratibu za lugha husika. Aidha, waasisi wa nadharia hii wanaeleza zaidi kuwa uradidi haufanyiki kiholela isipokuwa kuna mpangilio maalumu. Mpangilio huu hufanyika kulingana na taratibu maalumu zinazofuatwa katika suala zima la kupangilia kiradidiwa. Wanaendelea kufafanua zaidi kuwa kiradidiwa kinaweza kujitokeza kabla au baada ya shina au mzizi wa neno.

McCarthy na Prince (1993, 1994a, 1994b na 1995) waliitumia nadharia hii katika kazi zao kwani iliwaongoza kuonesha uelekeaji au uhusiano kati ya umboghafi na umbotokeo kulingana na kaida, sheria na taratibu za lugha zinazotafitiwa na wataalamu hawa. Mfano wa lugha waliyoifanya utafiti kuhusiana na mchakato wa uradidi ni lugha ya Axininca Campa (Hii ni lugha ya Kiarawakan) ambayo inazungumzwa nchini Peru. Nadharia hii ni muafaka katika makala haya kwani imetoa mwongozo wa nini kifanyike na kifanyike vipi ili kuepuwa upotoshaji wa maana pindi mchakato wa uradidi unapofanyika katika lugha ya Kihaya tunayoifanya utafiti. Aidha, kwa kuongozwa na nadharia hii, mtafiti aliweza kuhakiki usahili wa mchakato wa uradidi uliojitokeza katika vitenzi, vielezi na vivumishi nya Kihaya. Hivyo, mchakato wa uradidi umezingatia mfululizo wa viwango ambapo kila kiwango kimehusishwa na seti ya sheria za lugha hii.

Mbinu za Utafiti

Mtafiti wa makala haya anachunguza jinsi uradidi unavyojitokeza katika lugha ya Kihaya kwa kuangazia kategoria za vitenzi, vielezi na vivumishi. Ili kufikia malengo haya mtafiti ametumia mbinu kadhaa za kiutafiti. Kwa mujibu wa Kothari (1990) mbinu za ukusanyaji data ni mbinu zinazochaguliwa na mtafiti kwa lengo la kukusanya data ya utafiti wake. Kitchin na Tate (2000) wanaona kuwa kuchagua njia ya kukusanya data si kuchagua njia yoyote inayoonekana rahisi kustumia, bali ni kuchagua njia inayojitosheleza na inayohusiana na kile unachokitafiti. Utafiti huu umefanyika katika Mkoa wa Kagera, hususan katika Wilaya ya Muleba kata ya Izigo. Maeneo hayo yameteuliwa hasa kutokana na kuwapo kwa vyanzo vyta data inayohitajika kwa ajili ya makala haya kwani ndiko wazungumzaji wa lugha inayotafitiwa (Kihaya) inakozungumzwa. Pia ni vigumu kwa mtafiti kukusanya data kutoka katika maeneo mengi yenye wazungumzaji wa Kihaya kutokana na ufinyu wa muda na bajeti iliyopangwa kwa ajili ya utafiti huu. Kwa hakika maeneo yaliyoteuliwa yamewezesha upatikanaji wa data ya kutosha iliyotumika katika makala haya.

Ili kukusanya data ya makala haya mtafiti ametumia njia ya hojaji na chanzo cha data cha matabani. Hojaji ni orodha ya maswali na maelekezo yaliyoandaliwa na mtafiti ili yeweze kujibiwa na watafitiwa kwa lengo la kukusanya data ya utafiti. Njia ya hojaji iliteuliwa katika makala haya kwani njia hii humpa mtafitiwa uhuru wa kutoa majibu bila woga. Pia hojaji huweka ulinganifu wa majibu yanayotolewa na watafitiwa wote. Kutokana na njia hii, wazungumzaji wa Kihaya 20, (vijana 10, wa kike 5 na wa kiume 5, watu wazima 10, wanawake 5 na wanaume 5) walijaza hojaji ambapo mtafiti alihitaji orodha ya maneno yenye uradidi katika lugha ya Kihaya. Aidha, uteuzi wa idadi hii ya watafitiwa ulijumuisha wazungumzaji wa lahaja ya Kihamba ambayo ni lahaja mojawapo ya lugha ya Kihaya na ndiyo inayoshughulikiwa katika makala haya. Chanzo cha data cha matabani kilijumuisha usomaji wa nyaraka za kitaaluma kwa lengo la kupata data muafaka. Nyaraka zilizosomwa ni tasnifu mbalimbali, vitabu vinavyohusu uradidi unavyofanyika katika lugha mbalimbali na nyaraka mbalimbali za kitaaluma. Halikadhalika, data iliyokusanywa ilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli (usio wa kiidadi). Mkabala huu umetoa mwanya wa kuchanganua data kwa kutoa maelezo pasipo kubanwa na taratibu za kitakwimu. Makala haya yamelenga kuchunguza ni kwa namna gani uradidi unajitokeza katika kategoria ya vitenzi, vielezi na vivumishi katika Kihaya. Mtafiti anachunguza dhana hii kwa kina katika mjadala unaofuatia hapa chini.

Kategoria za Maneno

Hizi ni kategoria za kisarufi ambazo kwazo maneno ya lugha fulani huweza kuainiswa kulingana na uamilifu wake wa kisarufi na kimaumbo. Zipo aina kumi za kategoria za maneno ya Kiswahili ambazo ni: nomino, vitenzi, viwakilishi, vivumishi, vielezi, vihusishi, viunganishi, vihisishi, vionyeshi pamoja na vibainishi (Habwe na Karanja, 2004). Uradidi katika Kihaya hujitokeza katika kategoria za: nomino, vitenzi, vielezi pamoja na vivumishi. Mojawapo ya malengo ya makala haya ni kuchunguza ni kwa namna gani uradidi unajitokeza katika kategoria za vitenzi, vielezi pamoja na vivumishi katika Kihaya. Katika kipengele kinachofuata mtafiti anajadili dhana ya uradidi unavyojitokeza katika kategoria zilizobainishwa:

Uradidi katika Vitenzi

Vitenzi ni aina ya kategoria za maneno ambayo hutaja matendo. Kama ilivyo kwa kategoria nyinginezo, kama vile nomino, vielezi na vivumishi, uradidi pia hujitokeza katika kategoria ya vitenzi katika lugha ya Kihaya. Kitensi ni sehemu muhimu ya sentensi katika lugha yoyote ile, na ndiyo maana hata katika Kiswahili baadhi ya taarifa hutolewa kwa kitensi peke yake, mfano, amri kama *ondoka!*, *soma!* na *sema!* (Mnenuka, 2010). Katika lugha ya Kihaya, uradidi hujitokeza katika baadhi ya vitenzi na vitenzi vingine hughairi kupokea dhana hii. Tuchunguze vitenzi vinavyokubali mchakato huu wa uradidi:

Jedwali 1: Uradidi katika Vitenzi

| Safu A | | Safu B | |
|--|---|--|---|
| Kitenzi Ambacho Hakijaradidiwa katika Kihaya | Kitenzi Ambacho Hakijaradidiwa katika Kiswahili | Kitenzi Kilichoradidiwa katika Kihaya | Kitenzi Kilichoradidiwa katika Kiswahili |
| Abanafunzi <i>mbashoma.</i> | Wanafunzi <i>wanasoma.</i> | Abanafunzi <i>mbashomashoma.</i> | Wanafunzi <i>wanasomasoma.</i> |
| Abanakwaya <i>mbahoya.</i> | Wanakwaya <i>wanaimba.</i> | Abanakwaya <i>mbahoyahoya.</i> | Wanakwaya <i>wanaimbaimba.</i> |
| Ekigunjuk <i>kikakwata</i> omwana. | Mnyama <i>alimkamata</i> mtoto. | Ekigunjuk <i>kikakwatakawata</i> omwana. | Mnyama <i>alimshikashika</i> mtoto. |
| Embwa egi <i>nezala.</i> | Mbwa huyu <i>anazaa.</i> | Embwa egi <i>nezelazala.</i> | Mbwa huyu <i>anazaazaa.</i> |
| Juma <i>nagonza.</i> | Juma <i>anapenda.</i> | Juma <i>nagonzagonza.</i> | Juma <i>anapendapenda.</i> |
| Kokushubila <i>naleba.</i> | Kokushubila <i>anaangalia/anatazama.</i> | Kokushubila <i>nalebaleba.</i> | Kokushubila <i>anaangaliaangalia/</i> <i>anatazamatazama.</i> |
| Mwajuma <i>naandika.</i> | Mwajuma <i>anaandika.</i> | Mwajuma <i>naandikaandika.</i> | Mwalimu <i>anaandikaandika.</i> |
| Omukazi w'enda <i>nachwa</i> ebichwanta. | Mama mwenye mimba <i>anatemate</i> mate. | Omukazi w'enda <i>nachwachwa/nachwelel eza</i> ebichwanta. | Mama mwenye mimba <i>anatemate</i> mate. |
| Omumasai <i>akaguruka</i> n'ebyera. | Mmasai <i>aliruka</i> kwa furaha. | Omumasai <i>akagurukaguruka</i> n'ebyera. | Mmasai <i>alilukaluka</i> kwa furaha. |
| Omushabi <i>nashaba</i> amahela. | Oombaomba <i>anaomba</i> hela. | Omushabi <i>nashabashaba</i> amahela. | Oombaomba <i>anaombaomba</i> hela. |
| Omutamile <i>nagamba.</i> | Mlevi <i>anaongea.</i> | Omutamile <i>nagambagamba.</i> | Mlevi <i>anaongeaongea.</i> |
| Omwana <i>nayoga.</i> | Mtoto <i>anaoga.</i> | Omwana <i>nayogayoga.</i> | Mtoto <i>anaogaoga.</i> |

Chanzo: Data ya Uwandani, 2021

Data inayotumiwa katika makala haya inaonesha kuwa vitenzi vingi katika lugha ya Kihaya hukubali mchakato wa uradidi. Vitenzi vingi huhusisha uradidi kamili yaani kitenzi kizima kuradidiwa na baadhi huhusisha uradidi nusu yaani sehemu tu ya kitenzi huradidiwa. Kwa mujibu wa data ya makala haya vitenzi vifuatavyo vimepokea mchakato wa uradidi kama ifuatavyo: kitenzi *shoma* kimeradidiwa na kuwa *shomashoma*, *hoya-hoyahoya*, *kwata-kwatakawata*, *zala-zalazala*, *gonza-gonzagonza*, *leba-lebaleba*, *andika-andikaandika*, *chwa-chwachwa/chweleleza*, *gurukagurukaguruka*, *shaba-shabashaba*, *gamba-gambagamba*, *yoga-yogayoga*. Uradidi uliyojitokeza katika vitenzi hivi hudokeza tofauti ya maana kati ya vitenzi vilivyoradidiwa na vile visivyoradidiwa. Mathalani, kupunguza ukali au nguvu ya dhana husika, kuweka msisitizo, kudhoofisha maana, kuonesha kujirudiarudia kwa tendo nakadhalika. Hivyo, kila kitenzi kilichoradidiwa maana imebadilika kwa kiasi fulani. Kwa mfano tukiangalia vitenzi katika safu B katika jedwali letu, tunaona kuwa vitenzi vilivyoradidiwa, vinadokeza dhima zilizobainishwa hapo juu.

Uradidi Katika Vielezi

Vielezi ni maneno yanayotoa maeleo zaidi juu ya vielezi vingine, vitenzi, vivumishi au kuvumisha kategoria hizo. Kwa mfano, (a) Mwalimu anafundisha *taratibu*. (b) Mama yangu ni msafi *sana*. (c) Tutamaliza shule hivi *punde*. Katika sentensi (a) hapo juu, neno *taratibu* ni kielezi kinachovumisha kitenzi anafundisha. Katika sentensi (b) neno *sana* ni kielezi kinachovumisha kivumishi msafi. Aidha, neno *punde* katika sentensi (c) ni kielezi kinachovumisha kielezi kingine ambacho ni hivi. Baada ya kuona dhana ya vielezi kwa ufupi, tuone ni kwa jinsi gani uradidi unajitokeza katika aina hii ya kategoria katika lugha ya Kihaya.

Jedwali 2: Uradidi katika Vielezi

| Safu A | | Safu B | |
|---|--|--|---|
| Kielezi Ambacho Hakijaradidiwa katika Kihaya | Kielezi Ambacho Hakijaradidiwa katika Kiswahili | Kielezi Kilichoradidiwa katika Kihaya | Kielezi Kilichoradidiwa katika Kiswahili |
| Abagenyi baizile <i>bwankya</i> . | Wageni walikuja <i>asubuhi</i> . | Abagenyi baizile <i>bwankyabwankya</i> . | Wageni walikuja <i>asubuhiasubuhi</i> . |
| Adenitha naata <i>mpola</i> . | Adenitha anamenya <i>taratibu</i> . | Adenitha naata <i>mpolampola</i> . | Adenitha anamenya <i>taratibutaratibu</i> . |
| Anna nashoma <i>ge</i> . | Anna anasoma <i>vizuri</i> . | Anna nashoma <i>geigeige</i> . | Anna anasoma <i>vizurivizuri</i> . |
| Eishoke lya Kokubanza lishukile <i>kubi</i> . | Nywele za Kokubanza zimesukwa <i>vibaya</i> . | Eishoke lya Kokubanza lishukile <i>kubiikubi</i> . | Nywele za Kokubanza zimesukwa <i>vibayavibaya</i> . |
| Ekyalo kwa Ibwera kili <i>omunda</i> . | Kijiji cha Ibwera kiko <i>ndani</i> . | Ekyalo kwa Ibwera kili <i>omundamunda</i> . | Kijiji cha Ibwera kiko <i>ndanindani</i> . |
| Enjula negwa <i>muno</i> . | Mvua inanyesha <i>sana</i> . | Enjula negwa <i>munoimuno</i> . | Mvua inanyesha <i>sanasanana</i> . |
| Ensenene zagwa ¹ <i>zingi</i> . | Senene wamepatikana <i>wengi</i> . | Ensenene zagwa <i>zingizingi</i> . | Senene wamepatikana <i>wengiwengi</i> . |
| Mawe nalima <i>omungemu</i> . | Mama analima <i>migombani</i> . | Mawe nalima <i>omungemugemu</i> . ² | Mama analima kwenye shamba la migomba yenye ndizi ziliwazo tu na si aina nyingine ya migomba. |
| Mwalimu yaija <i>mwaha</i> . | Mwalimu amekuja muda <i>huu/sasa hivi</i> . ³ | Mwalimu amekuja muda <i>huuhuu/sasa hivi</i> . | Mwalimu yaija <i>mwahamwaha</i> . |
| Nimpandika <i>bwangu</i> . | Naandika <i>haraka</i> . | Nimpandika <i>bwangubwangu</i> . | Naandika <i>harakaharaka</i> . |
| Omwendo gwange ninguijwala <i>kileki</i> . | Nguo yangu nitaivaa <i>leo</i> . | Omwendo gwange ninguijwala <i>kilekikileki</i> . | Nguo yangu nitaivaa <i>leoleo</i> . |
| Rutinwa nayetaga ekyakulya <i>kyona</i> . | Rutinwa anahitaji chakula <i>chote</i> . | Rutinwa nayetaga ekyakulya <i>kyonakyona</i> . | Rutinwa anahitaji chakula <i>chochote</i> . |

Chanzo: Data ya Uwandani, 2021

Kipande cha data kilichopachikwa hapo juu kinaonesha kuwa vielezi ni mojawapo ya kategoria za maneno ambazo zina sifa kubwa ya uradidi. Hayo yanathibitishwa na data ya makala yetu: kielezi *bwankya* baada ya kufanyiwa uradidi kimekuwa *bwankyabwankya*, kielezi *mpola* kimefanyiwa uradidi na kuwa *mpolampola*, pia kielezi *ge* baada ya kuradidiwa tukapata kielezi *geigeige*, kielezi *kubi* baada ya kuradidiwa kimepatikana kielezi *kubiikubi*, halikadhalika, kielezi *omunda* kimeradidiwa tukapata kielezi *omundamunda*, kielezi *muno* pia kimefanyiwa uradidi na kuwa *munoimuno*. Uradidi umefanyika pia katika kielezi *zingi* ambacho kimejitokeza kama *zingizingi*, kielezi *omungemu* kimeradidiwa na kuwa *omungemugemu*, kielezi *mwaha* baada ya kuradidiwa

¹ Msamiati huu hauna kisawe chake katika Kiswahili.

² *Engemu* ni aina zote za migomba inayostawisha aina mbalimbali za ndizi. *Engemugemu* ni aina ya migomba istawishayo ndizi zilizokuwa zinaliwa na Wahaya toka enzi za mababu. Aidha, ndizi hizo (zitokanazo na *engemugemu*) ziliitwa: *enshakala*, *entobe*, *enfumbo*, *enchorcho*, *enyoya* nakadhalika. Siku hizi kuna aina nyingi za ndizi zinazoliwa na Wahaya isipokuwa ni tofauti na zile za zamani. Hizi hujulikana kama: *mutwishe*, *fia* na nyinginez. Pia zamani zilikuwepo ndizi za kutengenezea pombe na nyingine kuliwa zikiwa mbivu. Hizi ni kama: *enjoge*, *embiiile* na *obunana*.

³ Katika Kiswahili kielezi *sasa hivi* kinaghairi kuradidiwa tofauti na lugha ya Kihaya ambapo kielezi hicho huweza kufanyiwa mchakato wa uradidi.

kimejitokeza kama *mwahamwaha*. Aidha, kielezi *bwangu* baada ya kuradidiwa tumepata kielezi *bwangubwangu*, nacho kielezi *kileki* baada ya kufanyiwa uradidi tumepata kielezi *kilekikileki* na kielezi *kyona* kimejitokeza kama *kyonakyona* baada ya kufanyiwa uradidi. Aidha, imebainika kuwa baadhi ya vielezi hususan vile vinavyoolekea kurandana na vivumishi, mara nyingi hupunguza nguvu ya maana ya dhana inayozungumziwa pale vinaporadidiwa. Eneo jingine tulilolishughulikia katika makala yetu ni ujitokezaji wa uradidi katika vivumishi vya Kihaya kama inavyofafanuliwa hapa chini:

Uradidi Katika Vivumushi

Mojawapo ya malengo yetu ni kuchunguza ni kwa namna gani mchakato wa uradidi unajitokeza katika kategoria ya vivumishi katika Kihaya. Vivumishi ni vipashio ambavyo huvumisha nomino au viwakilishi kwa kutoa maelezo zaidi kuhusiana na nomino au viwakilishi hivyo. Mifano ya vivumishi ni kama vile: tukutu, stadi, yupi, ngapi, wale, hawa, bovu, safi, nne, saba, chache, nyingi, chetu, yangu nakadhalika. Tuangalie ni kwa namna gani mchakato wa uradidi hujitokeza katika vivumishi vya Kihaya:

Jedwali 3: Uradidi katika Vivumishi

| Safu A | | Safu B | |
|---|--|---|---|
| Kivumishi Ambacho Hakijaradidiwa katika Kihaya | Kivumishi Ambacho Hakijaradidiwa katika Kiswahili | Kivumishi Kilichoradidiwa katika Kihaya | Kivumishi Kilichoradidiwa katika Kiswahili |
| Abakola omutihani ni <i>bangi</i> . | Waliofanya mtihani ni <i>wengi</i> . | Abakola omutihani ni <i>bangibangi</i> . | Waliofanya mtihani ni <i>wengiwengi</i> . |
| Abanafunzi bashuntame <i>bashatu</i> . | Wanafunzi wakae <i>watatu</i> . | Abanafunzi bashuntame <i>bashatubashatu</i> . | Wanafunzi wakae <i>watatuwatatu</i> . |
| Egi emotoka <i>yange</i> . | Hili gari ni <i>langu</i> . | Egi emotoka <i>yangenyabwange</i> . | Hili gari ni <i>langu</i> kabisakabisa. |
| Enju <i>enke</i> yagwa. | Nyumba <i>ndogo</i> imeanguka. | Enju <i>enkenkenke</i> yagwa. | Nyumba <i>ndogondogo</i> imeanguka. |
| Entwiga eba <i>nda</i> . | Twiga huwa ni <i>mrefu</i> . | Entwiga eba <i>ndandanda</i> . | Twiga huwa ni <i>mrefu</i> sana. |
| Mwebesa <i>manzi</i> . | Mwebesa ni <i>shupavu</i> . | Mwebesa <i>manzimanzi</i> . | Mwebesa ni <i>shupavu</i> hasa. |
| Omwana <i>owawe</i> tiyakukwita. | Mtoto wako hawezi kukuua. | Omwana <i>owawenyabwawe</i> tiyakukwita. | Mtoto wako kabisakabisa/wa kumzaa hawezi kukuua. |
| Omwendo <i>gwikwela</i> gwanikile. | Nguo <i>nyeupe</i> imeanikwa. | Omwendo <i>gwikwelayela</i> gwanikile. | Nguo <i>nyeupenyeyeupe</i> imeanikwa. |
| Omwisiki <i>omurungi</i> niwe <i>yaija</i> . | Msichana <i>mzuri</i> ndiye aliyejuja. | Omwisiki <i>omurungirungi</i> niwe <i>yaija</i> . | Msichana <i>mzurimzuri</i> ndiye aliyejuja. |
| Tuguzile emotoka <i>mpya</i> . | Tumenunua gari <i>jipyा</i> . | Tuguzile emotoka <i>mpyapya</i> . | Tumenunua gari <i>jipyा</i> kabisa. |

Chanzo: Data ya Uwandani, 2021

Kutokana na data yetu, imebainika kuwa kategoria ya vivumishi katika lugha ya Kihaya hukubali kufanyiwa uradidi. Mifano iliyooneshwa katika Jedwali 3 hapo juu imethibitisha ukweli huu. Tuangalie vivumishi hivyo: kivumishi *bangi* kimefanyiwa uradidi na kuwa *bangibangi*, kivumishi *bashatu* pia kimefanyiwa uradidi na kuwa *bashatubashatu*, aidha, kivumishi *yange* baada ya kuradidiwa tumepata kivumishi *yangenyabwange*, kivumishi *enke* kimefanyiwa mchakato wa uradidi na kuwa *enkenkenke*, uradidi umejitokeza pia katika kivumishi *nda*. Kivumishi hiki kimefanyiwa uradidi na kuwa *ndandanda*. Halikadhalika, kivumishi *manzi* baada ya kuradidiwa tumepata kivumishi *manzimanzi*. Pia kivumishi *owawe* kimeradidiwa na kuwa *owawenyabwawe*. Mbali na vivumishi hivyo kufanyiwa mchakato wa uradidi, pia viro vivumishi mbalimbali vya Kihaya vilivyoonekana kukubali mchakato huu. Tuangalie vivumishi hivyo: kivumishi *gwikwela* baada ya kufanyiwa mchakato wa uradidi kimekuwa *gwikwelayela*, kivumishi *omurungi* kimekuwa *omurungirungi* na kivumishi *mpya* kimefanyiwa uradidi na kuwa *mpyapya*. Kutokana na mchakato

huu inaonesha kuwa uradidi huweza kujitokeza katika kivumishi kizima au sehemu tu ya kivumishi husika.

Hitimisho

Kwa ujumla makala haya yamechunguza ni kwa jinsi gani uradidi hujitokeza katika kategoria za Kihaya. Kategoria zilizoshughulikiwa ni: vitenzi, vielezi na vivumishi. Data ya makala haya inathibitisha kuwa uradidi hujitokeza katika kategoria tajwa kwenye lugha ya Kihaya. Matokeo ya makala haya, yamebainisha kuwa uradidi hujitokeza katika baadhi ya vitenzi na vitenzi vingine hughairi kupokea mchakato huu. Kwa vile lengo letu ni kushughulikia namna uradidi unavyojitokeza katika kategoria ya vitenzi na kategoria nyinginezo na si kuchunguza ni kwa namna gani vitenzi hughairi mchakato huu, hatukuangalia vighairi hivyo. Halikadhalika, matokeo ya makala yetu yanadhihirisha kuwa, vitenzi vingi huhusisha uradidi kamili ambapo kitenzi kizima huradidiwa na baadhi huhusisha uradidi nusu kwa maana kuwa sehemu tu ya kitenzi ndiyo hufanyiwa uradidi. Tofauti na kategoria ya vitenzi iliyoshughulikiwa katika makala haya, kategoria nyingine iliyoshughulikiwa ni kategoria ya vielezi. Vielezi ni mojawapo ya kategoria za maneno ambazo zina sifa kubwa ya uradidi katika lugha ya Kihaya. Matokeo yanaonesha kuwa baadhi ya vielezi hususan vile vinavyoelekea kurandana na vivumishi, mara nyingi hupunguza nguvu ya maana ya dhana inayozungumziwa pale vinapofanyiwa mchakato wa uradidi. Mbali na mchakato wa uradidi kujitokeza katika kategoria ya vitenzi na vielezi pia umejitokeza katika vivumishi vya Kihaya. Katika kategoria hii imebainika kuwa ama sehemu tu ya kivumishi au kivumishi kizima huradidiwa. Mtafiti amefanikiwa kuchunguza ujitokezaji wa uradidi katika kategoria za vitenzi, vielezi na vivumishi. Hivyo, makala haya yameonesha namna uradidi unavyojitokeza katika kategoria husika na hivyo kuchangia maarifa mapya katika lugha ya Kihaya kwani kwa mujibu wa makala yetu hakuna utafiti uliyokwishashughulikia eneo hili. Aidha, Kuna haja kubwa ya kufanya utafiti unaohusu dhana ya uradidi katika lugha ya Kihaya. Mathalani, ufanyike utafiti kuhusiana na namna uradidi unavyojitokeza katika kategoria nyingine kama vile nomino, vihusishi, vihisishi na viwakilishi. Aidha, utafiti ufanyike kuhusiana na dhima za uradidi katika Kihaya na lugha nyingine za Kibantu na zisizo za Kibantu ili dhima hizo zifahamike kwa wanaismu na wazungumzaji wa lugha husika.

Marejeleo

- Ashton, E.O. (1947). *Swahili Grammar (Including Intonation)*. London: Longmans.
- Bjorkman, B. M. (2009). "Uniform Exponence and Reduplication Evidence from Kinande". In *Spring 2008 Workshop in Phonology and Morphology*. 17mfm, May 30 2009: MIT.
- Downing, L. J. (2009). "Linear Disorder in Bantu Reduplication" In *Workshop on the Division of Labour between Morphology and Fourth Network Meeting*.
- Frawley, J. (2003). *International Encyclopedia of Linguistics*, Toleo la Tatu. Oxford, Oxford University Press.
- Habwe, J, na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Phoenix.
- Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam, TUKI.
- Kitchin, R, na Tate, N. (2000). *Conducting Research into Human Geography: Theory, Methodology and Practice*. United Kingdom: Pearson Education Limited.
- Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd Publishers.
- Lodh, A. Y. (2004). "Strategies of Emphasis and Intensity in Swahili". katika *Africa and Asia: Göteborg Working Papers on Asian and African Languages and Literatures*. No 4, 2004, kur. 142-150. Inapatikana katika <www.africanguse/aa/pdfs/aa04142pdf>; Ilisomwa tar. 14 Julai, 2021.
- Marcsik, E. A (1978). "Reduplicative Construction". In *Universals of Human Language*. Vol. 3. Word Structure Stanford University Press 1978: 299.
- McCarthy, J, na Prince, A. (1993). "Prosodic Morphology: Constraint Interaction and Satisfaction". In *Linguistics Department Faculty Publication Series*. Amherst: University of Massachusetts.
- McCarthy, J, na Prince, A. (1994a). "An Overview of Prosodic Morphology" OTS/HIL *Workshop on Prosodic Morphology*. Rutgers University.

- McCarthy, J, na Prince, A. (1994b). “The Emergence of the Unmarked: Optimality in Prosodic Morphology”. *Technical Report 32*, Rutgers University Center for Cognitive Science.
- McCarthy, J, na Prince, A. (1995). “Faithfulness and Reduplicative Identity”. *Papers on Optimality Theory*, 249-384. *GLSA, Amherst*, University of Massachusetts.
- Mnenuka, A. (2010). Dhima ya Uradidi katika Mawasiliano ya Kiswahili: Uimarishaji na Udhoofishaji wa Maana. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kswahili. Juz. 73 Uk. 32-44. Dar es Salaam: TUKI.
- Rubanza, Y. I. (1996a), “Dhana ya Uradidi katika Kiswahili”, katika *Jarida la Uchunguzi wa Kiswahili, Juzuu 59*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TUKI.

